Jiwe la kiroho la kujengea No. 112

# *WAKATI WA UKOMBOZI NI SASA*

*Waefeso 1:3-14; …..katika yeye huyo,(katika Yesu Kristo) kwa damu Yake, tunao ukombozi wetu,masamaha ya Dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake…. ……….."*

Na ukombozi un sehemu mbili tofauti."toka katika na "kuingia katika." Kwanza inabidi utoke nje . Watu wengine wanataka walete dunia pamoja nao; Lakini inabidi utoke katika ulimwengu ili kuingia ndani ya Kristo. Lazima utoke katika kutokuamini uingie katika Imani. Hakupaswi kuwe na kitu chochote katika njia yako. Kule kuwa na imani halisi, unapaswa kuacha kabisa nyuma,kila kitu ambacho kiko kinyume na Neno la Mungu ili kuingia katika imani.

Na "kukomboa," kunamaanisha, kurudishwa kule ulikokuwa nyuma." Unaona? Hawezi awakomboe wasioamini, haijalishi wana Elimu kiasi gani, na wana degree za udaktari walizo nazo. Hawezi kuwakomboa hao kwasababu hawawezi kukombolewa; lazima waende mahali pao. Wewe uliye ndani yake na ni sehemu yake kwa sababu ulikuwa sehemu katika mawazo yake. Kabla ya kuwekwa misingi ya dunia/ulimwengu, yeye alikuita wewe.(waefeso1:3-4; 2Tim1:9-10).

Makao yetu makuu yako mbinguni. Siendi Roma; ninaenda mbiguni ninapokufa, unaona? Ninaona. Makao makuu yako mbinguni.

Na mwili inabidi ufuate kichwa, kama vile mke amfuate mumewe. (yohana12:32) . Kwa vile Adamu hakudanganywa, akimfuata Hawa(Mwanzo1:22-24)Hawa alidanganywa. Akaingia katika hali ya kukosa, au vinginevyo ufufuo wa mwili wote ungekuja ungefanyika siku ile Bwana Yesu kristo, alipotoka kaburini, lakini ili amkomboe bibiarusi wake, ambaye ni mwili wake. Ilibidi akombolewe ndio aweze kuja kwake. Je unaliona hilo? Oh,jamani. Unaona? Isingewezakutokea wakati ule. Ukombozi ulikuwa unaendelea.

Sasa, unaona ile mihuri wakati ulipokuwa katika kiti chake cha rehema nyuma kule akikomboa? Lakini siku moja atakuja kuchukua kitabu kile alichokikomboa (ufunuo5:1-5), Na vyote vilivyomo ndani ya kile kitabu vimo ndani yake, na vyote vilivyomo ndani yake. Anakuja kwa ajili ya kitabu hiki cha ukombozi, ambao majina yao yaliandikwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia alipochinjwa kama kondoo.(ufunuo13:8;17:8). Na leo yuko hapa katika Neno lake, akidhihirisha kitu kile kile alichokifanya pale. Yeye(bibiarusi) hawezi kutambua kiongozi mwingine. Hapana, Bwana. Hakuna askofu, hakuna chochote. Yeye (Bibi Arusi) anatambua kiongozi mmoja tu; huyo ni Kristo; na Kristo ni Neno. Oh, jamani, wewe nalipenda hilo. Ndiyo Bwana.

Inaonyesha wazi kuwa wale tu waliochaguliwa kimbele ndio pekee wanaozungumziwa katika ukombozi umelipata hilo? Hebu niseme hilo tena. Wale tu waliochaguliwa kimbele ndio wanaofikiriwa katika ukombozi. Watu wanaweza kujifanya kama, wanafikiri wao ndio, lakini ukombozi wa kweli ni wale tu waliochaguliwa kimbele. Kwa sababu neno lenyewe "komboa" lina maanisha "kurejesha tena".
Hilo ni sawa? kukomboa kitu chochote ni kule kurejesha mahali pake pa awali. Haleluuuya. Kwahiyo ni kwa wale tu walio chaguliwa kimbele ambao watarudishwa tena mahali pao. Kwa sababu wengine hawakutokea hapo.

Lakini wale hasa waliochaguliwa na Mungu ile chembe halisi, ile chembe halisi ya uhai, ile nafsi ya Mungu ambayo ilikuwa ndani ya Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya dunia…… kumbuka, Ninyi ambao mmempokea kweli Roho wa Mungu ndani yenu, mlikuwa ndani ya kristo, kwa sababu yeye alikuwa ukamilifu wa neno. Alikuwa ukamilifu wa neno kwa jinsi ya mwili. Mungu alikuwa ndani ya kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake. (2kor.5:18-19). Unaamini hilo? Angalia, yeye alikuwa ndani ya kristo. Sasa kama ulikuwa ndani ya Mungu, ile chembe, neno, sehemu ya Mungu tangu mwanzo, halafu ulitembea Naye hapa duniani, ulizunguka Naye hapa duniani, uliteswa pamoja Naye hapa duniani,ulikufa pamoja Naye pale msalabani; na ulifufuka pamoja Naye tena; na sasa umeketi pamoja na Kristo Yesu katika ulimwengu wa kiroho, ukizungumza Naye, kadiri unavyolisha nafsi yako, kwamba, "mtu ataishi kwa kila Neno litokalo…….."

Kwa hiyo unaona, kama ulikuwa katika ufahamu wa kimbele wa Mungu, hivyo unakuwa sehemu ya Mungu. Na njia pekee uwezayo kuwa mwana wa Mungu au binti wa Mungu, lazima uwe sehemu ya Mungu, na Mungu hakukamilika bila wewe. Lazima uwe hivyo. Hiyo ni kweli. Kwa sababu kuna moja, njia moja tu chimbuko la uzima wa milele, na hilo ni Mungu. Na Yeye pekee anao uzima wa milele.

Unaona? Sasa, na ulikuwa sehemu yake, kiasi kwamba u sehemu yake, au katika mawazo yake pale mwanzo. Na kwa sababu Alikuwaza wewe tangu pale mwanzo, inatoa ule mvuto mdogo kumuelekea yeye. Hicho ndicho kinacho huishwa. Wengineo hawawezi kamwe kuhuishwa; maana hawana hicho; hivyo tu.

Kama vile kichwa kilivyoinuliwa toka kaburini, kadhalika mwili wake lazima umfuateYeye kule Edeni. Kwa hiyo mwili hauwezi kutambua kichwa kingine, ila kichwa cha Neno. Hakuna dhehebu liwezalo kuweka chochote kwa hilo.

Lakini unaona, katika hiki kitabu kipo kile kilicho kombolewa; kilikuwa kitabu cha ukombozi. Na kila alicho kikomboa kilikuwa kimeandikwa katika hicho kitabu. Vyote alivyo vifilia vilikuwa vimeandikwa katika hicho kitabu, na asingeweza kuondoka katika kiti cha rehema mpaka awe amekwisha kukomboa kikamilifu, na asingeweza kukikomboa pale msalabani, kwa sababu alichaguliwa kimbele katika kitabu cha uzima cha mwana kondoo, na ilibidi akae pale ili afanye upatanisho mpaka mtu wa mwisho awe amemaliziwa. Utukufu.

Neema imezaa utu wa Yesu kristo. Mungu alitandaza hema yake, alitoka kwa Mungu kuwa mwanadamu. Alibadili hali yake kutoka Mungu mwenyenzi akawa mtu, akachukua hali ya ubinadamu, ili aweze kufa awakomboe wanadamu (wafilipi 2:5-11). Subiri mpaka tumuone yeye wakati hakuna yeyote anayestahili. Unaona?

Na Mungu, muumbaji wa roho, alikuwa ndugu wa karibu kwetu alipochukua umbo la kibinadamu ili aweze kuchukua dhambi zetu juu Yake, na kulipa deni, na kutukomboa kuwa wa Mungu tena.

Asinge pumzika mpaka alipoilipa deni kamili ya ukombozi ili kukukomboa wewe, kila kitu alicho wahi kupoteza, kila kitu ulichokuwa.

Hili hapo. Yule pale Mkombozi. Kristo amekukomboa sasa (waefeso 1:7-8). Sasa tumekombolewa, lakini Hajadai haki ya umiliki wake bado. Sasa, unaweza usikubaliane na hilo, lakini tulia kwa dakika; tutaona. Unaona?

Na alifanya nini sasa? Alikuwa nyuma pale akifanya upatanisho mpaka Damu yake imemuosha kila mtu, na mwana kondoo sasa, anajua kilicho andikwa kitabuni, (1yohana.2:2) kwa hiyo alijua kutoka kuwekwa misingi ya dunia kuwa majina yao yako pale, kwa hiyo alisimama nyuma pale na kufanya upatanisho kama hivi mpaka kila mmoja ambaye ameandikwa katika kitabu amekombolewa na imekwisha, na sasa anaondoka kwenye kiti cha rehema.

Yeye bado hajalidai hilo. Unaona? Kama umechukua kitabu cha ukombozi, kila kitu alichokuwa nacho Adamu na kila kitu alichopoteza, Kristo amekikomboa na kukirudisha, na Yeye tayari ametukomboa sisi, lakini yeye bado haja vichukua kama mmiliki wake bado. Hawezi mpaka wakati ulioamriwa, na baada ya hapo unakuja ufufuo (ufunuo 20:6) na hapo sasa dunia itafanywa upya tena, na halafu yeye atachukua umiliki, umiliki wake ambao alimpata pale Alipotukomboa sisi, lakini atalifanya hilo kwa wakati ulioamriwa. Oh;mimi.

Sasa ile siri ya kitabu inafunuliwa wakati mihuru inapovunjwa. Na wakati mihuri imevunjwa kikamilifu, wakati wa ukombozi utakuwa umekwisha, kwa sababu Mwanakondoo ataondoka mahali pa upatanisho na kwenda kule kuchukua madai yake. Yeye alikuwa mpatanishi katika hilo,, lakini wakati ufunuo halisi utakapotokea kuhusu hii mihuri, vile inavyo anzakuvunjwa, Mwana kondoo anakuja kutokea madhabahuni. Hiyo ni sawa na neno. (hiyo ni sawa yeye alikuwa mpatanishi) Anakuja kutoka katikati ya (kiti cha enzi) na kuchukua kitabu (ufunuo5:6-7). Kwa hiyo yeye siye mpatanishi tena, kwa sababu hata walimwita yeye ni simba, na huyo ni Mfalme, na Yeye siyo mpatanishitena.

Hiyo siri ilikuwa ndani ya (moyo) Mungu miaka hii yote ikiwa imefunikwa na mkono wake wa kuume, Yesu. Yule mchungaji mkuu ambaye alichukua juu yake maovu yetu sisi Isaya53:5 alisema, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya Amani yetu ilikuwa juu Yake. Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona”. Siri ya Mungu ya uponyaji ilikuwa moyoni ya Yesu kristo, oh Mungu. Yeye alikuwa mkono wa kuume wa Mungu; huyo ni kondoo pekee aliyekuwa ameshikilia katika moyo wake ile siri. Hiyo ndiyo maana kivuli cha utangulizi wa hilo siku zote ilikuwa ni kondoo. Wa kwanza alikuwa ni kondoo (Mwanzo3:21); wa mwisho alikuwa kondoo. Hiyo ndiyo sababu ilibidi Yeye kuwa Mchungaji, ilikujua namna ya kumhudumia kondoo wake. Unalipata hilo? Angalia, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu,Adhabu ya Amani yetu ilikuwa juu yake”.

Na wakati Mchungaji mkuu, yule kondoo nabii, Aliposema………. Pale msalabani, Alipokuwa amelipa adhabu ya dhambi kwa ajili yetu sote, Alisema, “Imekwisha” (yohana19:30). Dhambi ilikwisha, adhabu

imelipwa, deni lilimalizwa. Haikuchukua mwaka, au baadaye likaja katika siku za watengenezaji au kitu Fulani; ilikuwa, ilimalizika palepale.

Dhambi iliingia mara moja kwa uvunjaji wa sheria za Mungu, Kwa kuvunja Neno moja. Usiku wa leo, ndugu zangu, nafsi yako imening'inia kuzimu katika mnyororo. Na huo mnyororo siyo mafundisho ya theolojia ya seminari fulani, siyo dhehebu fulani au kanuni fulani upaswayo kuishi kwayo; Nyororo hiyo ni neno la Mungu. Yesu aliupa uzao wa wanadamu waishi kwa neno lake na Hawa alivunja sehemu ndogo tu ya hiyonyororo. Na nyororo yote nguvu yake iko katika kiungo kile kidhaifusana.Unapoondoa neno moja nje…….

Na dakika hiyo, mara huyo mchungaji anapopigwa, ilikuwa, imekwisha. Dhambi ilikwisha; hakukuwa na dhambi tena. Walikuwa safi; adhabu ililipwa. Waaminio ambao majina yao yalikuwa yameandikwa katika kitabu cha uzima, waliochaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ilikuwa imekwisha dakika ile Yesu aliposema imekwisha. Yeye, yule Mchungaji mkuu, alikuja kwa ajili ya kondoo wake. Ilikuwa imekwiha.

Wewe ni mkristo unayo haki kwa kila baraka ya ukombozi ambayo Yesu alikufa kwa ajili ya hiyo iwe yako. Zote ni zako. Zimeshalipiwa; lazima uamini hilo, siyo ya kuwazia, bali kuliamini, na kujua kwamba ni yako, na unaweza ukaimiliki hiyo.

Nukuu: za kiingereza
(1)Mungu aliye mwingi wa rehema; aya30
(2)Kuthibitisha Neno lake, aya 209
(3)Kristo ni siri ya Mungu iliyo funuliwa, aya242-245
(4) Huyu Melkizedeki ni nani?; aya 116
(5)Matukio yakiwekwa wazi na unabii ( 65-1206) Aya 17
(6)Nafsi zilizo kifungoni sasa uk 24
(7)Lile pengo, Aya 85-89,140
(8)Ule muhuri wa tatu Aya 169
(9)Muhuri wa kwanza Aya 29,
(10)Kwa nini iwe ni wachungaji Aya 176-183
(11)Imani kamilifu Aya 146.

*jiwe la kiroho la kujengea na 103. kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*
*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*
*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*